


Word of Faith Int'l Christian Center

# 30 Days of Prayer

## Siku Thelathini za Maombi

---

**Januari 02 – Januari 31, 2024**

pray30.org • #pray30

## BISHOP KEITH A. BUTLER

Senior Pastor and Presiding Bishop
Word of Faith Southfield, MI

### Siku ya Kwanza – Liombee Taifa Lako

Karibu kwa siku thelathini za maombi. Tuanzie kwanza kabisa kutoka barua ya Paulo kwa Timotheo katika Timotheo wa kwanza; sura ya pili, mstari wa kwanza. Inasoma, "Basi kabla ya mambo yote, nataka dua [ ombi la uhakika], na sala…" Kuna aina nyingi za maombi. "maombezi," – kuwa tayari kusimama kwenye pengo kati ya Mungu na pengine mtu binafsi anayehitaji usaidizi. "na shukrani," – kwa sababu kila wakati unapoomba, unajua kuwa Mungu hulisikia ombi lako. "kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme wote, na wote wenye mamlaka;" Hili neno mamlaka linamaanisha wale walio katika nyadhifa za juu. Sasa, kwa yale yote yanayofanyika duniani – vita vinavyofanyika sasa hivi – angalau mbili yavyo – na mambo mengine yanayofanyika kwa wakati huu - huu ni wakati tunaopaswa kuomba haswa kwa wale walio mamlakani. Hao ni rais na Bunge. Kwa sababu ya viongozi wa mataifa walio kwenye vita. Kwa sababu ya viongozi wa biashara. Kwa sababu ya wale wanaohusika katika kuathiri maisha yetu yote.

Kumbuka inavyosema hapa: "Kwa ajili ya wafalme, na wote wenye mamlaka;" Kwa sababu maamuzi yanayofanywa hutuathiri sisi sote, ikiwa unaongea kuhusu bodi za shule au unaongea kuhusu mashirika maalum – lakini maisha yetu yote huguswa na watu walio kwenye nyadhifa za juu. Maisha yetu yote huguswa na watu walio mamlakani. Hio ndio maana tunabarikiwa tunapokuwa na fursa ya kuchagua watu hawa ni akina nani. Ni muhimu sana.

Tusome aya iliyobaki. Tukiwaombea, "tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu." Kwa maneno mengine, badala ya hila na ajenda zilizofichwa na mambo haya mengine yote, mambo yanaweza kuwa ya wazi na Neno linatuambia kuwa kanuni za kimungu zitakuwa kuu kwa siku kwa sababu Mungu anapata kufanya kazi duniani. Mungu anafanya kazi duniani kwa sababu watu humuuliza

Katika maandishi katika Isaya, wana wa Israeli walipojitia kwenye shida na Mungu, Biblia inasema kuwa Mungu alishangaa kuwa hakukuwepo mwombezi – hakukuwa na mmoja wa kusimama kwenye pengo kati Yake na Israeli yenye dhambi. Maombezi ni muhimu. Maombi kwa ajili ya walio mamlakani ni muhimu. Kisha inaendelea kusema katika mstari wa tatu, "Hili ni zuri nalo lakubalika…" Ni lipi linalokuabalika? Kuwa tuishi maisha ya utulivu, maisha ya amani, maisha yaliyojaa utauwa, na ustahivu. Na kisha mstari wa nne, "Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli." Neno la Kigiriki la maarifa ni epignosis – utambuzi kamili, ufahamu kamili wa ukweli ni nini, kinyume na uongo mwingi tunaoshughulika nao. Kwa hivyo asante sana kwa kuhusika katika siku thelathini za maombi. Maombi yako yataleta mabadiliko duniani. Mungu akubariki.

**PASTOR JEAN KINUTHIA**
Senior Pastor • Faith4Life
Nairobi, Kenya

## Tuombee Umoja na Ushirika katika Mwili wa Kristo

Jambo. Jina langu ni Jean Kinuthia, Mchungaji Mkuu, Kanisa la Faith4Life, Nairobi, Kenya. Karibu kwa siku ya pili ya siku thelathini za maombi.

Leo tunaombea umoja na ushirika katika mwili wa Kristo. Zaburi 133, mstari wa kwanza na wa pili inasoma hivi, "Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, Ndugu wakae pamoja kwa umoja! Ni kama mafuta mazuri kichwani, yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake;" Mstari wa pili unaelezea athari za ndugu kuishi pamoja kwa amani. Kulikuwa na ule mtiririko usiokatika wa upako huo. Tazama, umoja huruhusu mtiririko usiokatizwa wa nguvu za Mungu, wa upako wa Mungu, wa kazi ya Mungu, kupitia kwa mwili wa Kristo. Ninaifikiria kama bomba ambalo hubeba yaliyomo kutoka mwisho mmoja hadi mwingine. Lakini ni nini hufanyika bomba linapopasuka? Utayapoteza yaliyomo, sivyo? Basi, hiyo ni sawa na nguvu za Mungu. Umoja na ushirika vitaendeleza mtiririko wa nguvu na kazi Yake; ilhali utengano, ugomvi na kutosamehe huvunja mtiririko huo. Kwa hiyo tutaendeleaje kuwa wamoja?

Katika Waefeso sura ya nne, mstari wa kwanza, Maandiko yanatuambia tuenende kama inavyoustahili wito wetu tulioitwa. Na kwa mstari wa pili, tunapata majibu ya swali – tutafanyeje mwenendo huo inavyostahili? Unatupa jibu la swali tunalouliza - tutakaaje kwenye umoja wa imani? Hivi ndivyo inavyosoma, "Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo;"

Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya badala ya ugomvi na kutosamehe. Labda hiyo ni sehemu ya yale mimi na wewe tunayoomba kwa ajili ya kila mmoja wetu katika mwili wa Kristo kwamba badala ya kujibu kwa kimwili, tukiangalia kulipiza kisasi, kwamba tunyenyekee na kushughulika sisi kwa sisi kwa upendo, katika saburi, katika uvumilivu, katika uthabiti. Labda sehemu ya vile tunavyoomba leo ni kuuliza Mungu atusamehe wakati hatujafanya hivyo.

Mstari wa tatu unasoma hivi, "Na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani." Kwa hivyo, tuna bidii ya kulinda amani. Tuna bidii ya kubaki katika kifungo hicho cha amani sisi kwa sisi. Katika Sala la Bwana katika Yohana Sura ya kumi na saba, Yesu aliomba kuwa tuwe wamoja kama vile Yeye na Baba ni wamoja. Umoja huu uliruhusu uwezo na nguvu na mpango wa Mungu kukamilishwa kupitia Kwake. Hivyo tuombee umoja na ushirika katika mwili wa Kristo leo.

**PASTOR MATTHEW TARKINGTON**
Senior Pastor • Faith4Life
Dallas, Texas

## Ombea Familia Yako na Marafiki Wako

Unachukulia nini kuwa jukumu lako kubwa- jambo la muhimu zaidi maishani mwako? Ni kazi yako, cheo chako kanisani, wajibu wako kwa nchi yako? Habari, jina langu ni Mchungaji Matt. Mimi ni Mchungaji hapa katika Kanisa la Faith4Life hapa Dallas, Texas.

Biblia hutuambia kuwa jukumu letu kubwa zaidi letu ni kwa husiano alizoweka Mungu maishani mwetu, haswa kwa familia zetu na marafiki. Sasa, tunaweza kuzungumza kwa saa moja kuhusu mambo tofauti tunayoweza kuombea kuhusu familia na marafiki. Lakini leo tutaongea tu kuhusu mambo matano na yanatamka neno FAMILIA (FAMILY).

Kwanza ni herufi F. Tutaombea Imani (Faith) yao. Yoshua 24:15 husema, "lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana." Tutaenda haswa kuwaombea wanafamilia na marafiki ambao hawajafanya uamuzi wa Kristo kuwa Bwana wao waufanye uamuzi huo na wale ambao wamefanya uamuzi wawe imara katika imani yao.

A – ni tutaenda kuombea mtazamo (Attitude) wao. Waefeso 6:1-3 inasema, "Enyi watoto, waheshimu baba yako na mama yako." Kisha kwa mstari wa nne inasema, "Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu." Tutazungumza kuhusu mtazamo na kuomba kwa ajili ya mitazamo ya familia na marafiki kuwa wawe na heshima mmoja kwa mwingine na kwa Bwana.

Kinachofuata ni M. Tutaenda kuombea pesa zao (Money). Omba Baraka zilizo katika Kumbukumbu la Torati ishirini na nane juu ya familia yako na marafiki wako, kuwa wao ni kichwa wala si mkia, watakuwa juu tu, wala hawawi chini – kuwa wamebarikiwa mjini na wamebarikiwa mashambani.

Na tutaenda kuombea I – Yaani utambulisho (Identity). Katika Timotheo wa kwanza sura ya tatu, mstari wa pili hadi wa saba, inaongea kuhusu Askofu jinsi anavyopaswa kuwa mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja. Lazima awe mkaribishaji. Kisha inaendelea kuongea katika mstari wa saba kuwa ana jina jema nje. Inamaanisha utambulisho anaojulikana nao, watu wengine wanaweza kumsherehekea na kumuunga mkono. Omba kwa ajili ya utambulisho wa wanafamilia wako.

L – tutaenda kuwaombea matembezi yao ya upendo (Love). Wagalatia 5:6 husema kuwa imani hutenda kazi kwa upendo. Hiyo inamaanisha kuwa tunapaswa kuwa tunaomba kuwa waendelee kusimama imara katika matembezi yao ya upendo.

Na ya mwisho ni Y – na tutaenda kuomba kuwa wawe na mioyo ya kujitoa (Yielding), kuwa waisikilize sauti ya Roho Mtakatifu na wamfuate kila wakati. Tuombe pamoja.

**BISHOP BETHEL CHOTO**
Word of Faith Miracle Christian Ministries
Pretoria, South Africa

## Ombea Uhuru wa Kuabudu

Shaloma familia. Jina langu ni Askofu Bethel Choto, nikiongea kutoka Afrika Kusini. Leo ni siku ya nne ya maombi yetu. Tunaombea uhuru wa kuabudu. Tafadhali tufungue Bibilia zetu katika Wathesalonike wa pili sura ya tatu, mstari wa kwanza. Na inasoma hivi, “Hatimaye, ndugu, tuombeeni, neno la Bwana liendelee, na kutukuzwa vile vile kama ilivyo kwenu:” Na pia Yohana wa kwanza sura ya nne, mstari wa nne, inasoma hivi, “Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.”

Leo tunaombea haki yetu kama kanisa kumwabudu Yesu Kristo. Shetani anajenga miundo akijaribu kukandamiza haki zetu kuu za uhuru wa kuabudu. Tuna mamlaka juu ya chochote ambacho Shetani anaweza kujaribu. Maombi yetu ni muhimu sana wakati wa mashambulizi. Maombi huuwezesha ujumbe wa Ufalme wa Mungu kuhubiriwa bila ya adui kusimamisha kanisa.

Mwisho, na tujiunge pamoja kwa imani yetu ili ujumbe wa Yesu Kristo na utukufu Wake uendelee kuenea kwa kasi na utambulike kote ulimwenguni. Tunaomba kuwa Mungu ataliokoa kanisa kutoka kwa mashambulizi ya watu waovu walio nyuma ya kutunga sheria na taratibu zinazotaka kuuchukua uhuru wetu wa kidini.

Mwisho, na tujiunge pamoja kwa imani na kila muumini kwamba tunajiamini na tuko na uhakika kabisa kwamba sisi ni wa Mungu na tu wana wake na tumewashinda walio duniani kwa kuwa Aliye ndani yetu ni mkuu kuliko yeye aliye duniani. Maarifa haya yanatufanya kusimama wima bila uwoga. Tuombe katika Jina la Yesu.

## PASTOR MICHELLE FERGUSON

Executive Pastor • Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

### Omba Kwa Ajili ya Afya Yako na Fedha Zako

Habari. Karibu kwa siku ya tano ya siku thelathini za maombi. Mimi ni Mchungaji MiChelle Ferguson na leo tutaombea afya yetu na fedha zetu. Nataka kuanza kwa kwenda katika Petero wa kwanza sura ya pili mstari wa ishirini na nne ambao unasema, "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."

Kama mtu aliye na ushuhuda baada ya ushuhuda, kuwa Mungu bado hujibu kwa moto leo – kuwa nguvu ya Mungu ya kuponya bado iko hai na sawa, nataka kuwakumbusha kuwa andiko hili linaongea kuhusu- sio kwamba tumeponywa; bali ni kuwa tuliponywa. Kila bei iliyohitaji kulipwa kwa uponyaji wako ilishalipwa tayari. Hivyo sijali kile ambacho umekuwa ukikipitia. Sijali anachosema daktari, utambuzi ni upi, au hata unavyojisikia. Damu ya Yesu iko hai na sawa na inatenda kazi ndani ya mwili wako. Hivyo tunataka kuendelea kuombea hilo. Na pia, fedha zetu.

Unajua, mojawapo ya mambo kuhusu uponyaji ni kuwa kwa watu wengi ambao wameupitia, na hata katika ushuhuda wangu mwenyewe, Shetani wakati mwingine atazitumia changamoto za kiafya hata kuzipunguza fedha zako. Kwa hivyo ni wakati mzuri sana wa kujumuika na hilo. Malaki sura ya tatu, mistari ya kumi na kumi na moja inazungumza kutoka umuhimu wa kuleta zaka kamili ghalani na jinsi Mungu atakavyofungua madirisha ya mbinguni na kumkemea yeye alaye, kwa niaba yetu.

Hiyo inamaanisha nini? Hiyo inamaanisha kuwa Shetani hana haki. Wewe ni mtoaji. Wewe ni mwaminifu kuwa na mkono Wake kwa kitabu chako cha mfukoni, mkono kwa maisha yako, na kuweza kutoa alichokubariki Mungu nacho. Hivyo tunataka kuchukua mamlaka juu ya hio. Na nataka kumalizia kwa kukukumbusha Wafilipi sura ya nne mstari wa kumi na tisa, inasema hivi, "Na Mungu wangu atawajazeni kwa kadri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu." Hivyo leo tujumuike pamoja, twende mbele ya Bwana kwa maombi tukizingatia maeneo haya mawili ya maisha yetu sio tu ili tukae starehe - ili tupate -lakini kuwa Mungu, kupitia kwetu, anaweza kuwabariki wengine.

**MINISTER KRISTINA JENKINS**
Word of Faith International Christian Center
Southfield, Michigan

## Waombee Wachungaji Wetu na Viongozi wa Kiroho

Karibu tena kwenye siku thelathini za maombi. Mimi ni Mtumishi Kristina Jenkins na leo tutawaombea wachungaji wetu na viongozi wa kiroho. Nataka kukusomea leo kutoka Wakolosai sura ya nne, mstari wa kumi na mbili na unasema, "Epafra, aliye mtu wa kwenu, mtumwa wa Yesu Kristo, awasalimu, akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi yake, ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu." Je wajua kwamba uongozi wa kiroho kweli ni wazo la Mungu? Katika Yeremia, Neno la Mungu linasema, "Na nitawapa wachungaji wanipendezao moyo Wangu ambao watawafunza na kuwalisha maarifa na ufahamu." Na sio hilo tu, ametupa sisi, kama mwili wa Kristo, jukumu la kushikilia juu mikono ya uongozi wa kiroho. Jambo kubwa kuhusu hilo ni kuwa sio tu la faida kwetu kuwainua wachungaji wetu na viongozi wa Kiroho kwa sababu tunawapenda na kuwajali, bali hata inakuja kweli na kutufaidi kwa sababu tunaendelea kuwaombea kwa bidii mara kwa mara, inawasaidia kutenda kile ambacho Mungu amewaita kufanya, ambayo kama tulivyosoma hapo punde kuhusu wachungaji wetu ni kusaidia kuhakikisha kuwa tumefunzwa hekima na ufahamu na kuwa roho ya mchungaji imefungamana na roho ya Mungu.

Na kwa hivyo leo nataka kukuonya na kukuhimiza. Ningetaka kukuhimiza vilevile usome Waefeso sura ya kwanza, mstari wa kumi na sita hadi wa ishirini na moja kabla tuombe leo ili ujue na utambue kuwa Mungu ametupa uletaji wa Roho Mtakatifu ili tuweze kuombea viongozi kwa kingereza na ndimi zingine, na tuwaombee kuwa wataweza kukamilisha mapenzi ya Mungu – kuwa watatembea wanaostahiki wito walio nao – kuwa wawe na shina na msingi katika upendo na wapate kufahamu ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina cha upendo wa Yesu Kristo pamoja na sisi wote na watakatifu wote kwa sababu hio inatusaidia sisi wote kuwa na ufanisi kwa kile alichotuita Mungu kufanya. Na tunapowainua viongozi wetu wa kiroho leo, tufanye hivyo kwa ujasiri, tufanye hivyo kwa bidii tukijua kuwa tumeteuliwa na kuandaliwa kufanya hivyo, na kama matokeo ya maombi yenu, wachungaji wetu wataweza kukamilisha mpango wa Mungu kwa maisha yao na watusaidie kuukamilisha mpango wa Mungu kwetu.

## PASTOR RAY MCCLINTOCK

Word of Faith Int'l Christian Center
Soutfield, Michigan

### Waombee Wanaojitolea katia Kanisa Lako

Habari. Mimi ni Mchungaji Ray McClintock kutoka makao makuu ya kanisa hapa Southfield, Michigan.

Ni heshima kuu kwangu kuwaletea siku ya saba ya siku thelathini za kampeni ya maombi. Nimekuwa kwa huduma ya wakati wote kwa muda wa miaka ishirini na waume, na wake wote ninaowajua kwa huduma walianzia katika huduma ya usaidizi. Kama unataka kumfanyia Mungu jambo kubwa, nina mahali mwafaka pa kuanzia na hapo ndipo mwanzo wa huduma zote – huduma ya masaidiano. Maandiko hutuambia tusipuuze siku za mwanzo mdogo. Nakumbuka nikiwa Shule ya Biblia, nikiwa pia kwenye huduma ya masaidiano. Kwa hivyo nilipokuwa nikijifunza kuwa mtumishi mwaminifu wa Mungu, nilikuwa pia na nafasi ya kutumia ujuzi huu wa kuwa mtumishi mwema.

Tazama, Yesu alikuwa kiongozi mtumishi mkamilifu. Ikiwa unatazamia kuanza ujenzi, utaanza kama kibarua. Ikiwa ungependa kuingia katika biashara, unaweza kuanza kama karani. Hizi ni sehemu za kuingilia katika maeneo ya huduma. Ikiwa unatafuta sehemu za kuingilia katika maeneo ya huduma, kuna nyingi ambazo zote huwa chini ya kichwa cha masaidiano. Zote hufanya kama vile linalosema jina - zinasaidia.

Wakati mwingi, huna maarifa wala ufahamu mwingi, lakini kuwa tu tayari kumsaidia mwanamume au mwanamke mwingine kuwa mwaminifu kwa eneo hilo maalum la huduma. Unaanza kwa maombi ili kutambua mahali ambapo utatumikia katika huduma ya masaidiano.

Katika Wakorintho wa kwanza sura ya kumi na mbili, mstari wa ishirini na saba hadi thelathini na moja inasema hivi, "Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha. Je! wote ni mitume? Wote ni manabii? Wote ni waalimu? Wote wanatenda miujiza? Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote watafsiri? Takeni sana karama zilizo kuu. Hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora." Tambua kuwa katika mstari wa ishirini na nane haujiweki mwenyewe, lakini anayekuweka ni Mungu. Hivyo, kama tayari wewe si mtumishi katika huduma ya masaidiano, na tufungue mlango kwa maombi ili Mungu akuweke mahali unapostahili, kuusaidia mwili wa Kristo kwa kuanza safari hii kumfanyia Mungu mambo makuu. Kwa hivyo, mtumishi mwema na mwaminifu, jua kuwa Askofu na Mchungaji Deb wanakupenda na hukuombea. Huyu ni Mchungaji Mack nikisema, "Mungu akubariki," kutoka makao makuu ya kanisa na ninatarajia kutumikia kando yako kwenda mbele.

## PASTOR KERRICK BUTLER

Senior Pastor • Faith Christian Center
Austell, Georgia

### Ombea Udhihirisho Mkubwa Zaidi wa Zawadi za Roho

Habari. Mimi ni Kerrick Butler kutoka Faith Christian Center. Asante kwa kujumuika nasi katika siku thelathini za maombi. Maisha yako ya maombi ni muhimu. Uambazaji wa maombi yako ni muhimu. Hivyo basi twendelee kuomba pamoja kwa sababu tunajua kuwa Mungu anaweza kufanya mambo makubwa yafanyike kupitia kuomba kwetu kwa sababu tunajua kuwa maombi huzalisha nguvu kuu za ajabu.

Leo nataka kukuhimiza uombee udhihirisho mkubwa zaidi wa zawadi za Roho. Zawadi za Roho sio tu moja kwa moja ukisema, "Kama Mungu anataka itendeke, itatendeka moja kwa moja." Sasa, hii ni sehemu ndogo pekee, kwa sababu Mungu ni mwenye enzi lakini ameelekeza tutamani zawadi hizi. Hamu, maana yake inamaanisha kutaka, kutamani. Hata kwa Kigiriki inamaanisha kutamani. Hiyo inamaanisha inakupasa kufuata kwa nguvu zawadi za Roho. Na njia moja ya kufanya hivi ni kupitia maombi- kwa kumuuliza Mungu atupe udhihirisho mkubwa zaidi wa zawadi za Roho Mtakatifu. Sio tu kusema, "Ikiwa Mungu anataka kuwahudumia watu, atawahudumia." La. La. La. Anataka tushirikiane naye kwa maombi pale zawadi za Roho zinapohusika. Kwa hivyo hapa kuna baadhi ya mambo ambayo unapaswa kuyaombea. Ombea ububujiko huru wa zawadi za Roho kote kwa ibada na kusanyiko unazoweza kuwa ukihudhuria katika kanisa lako, bila shaka, na mikutano mingine.

Unataka kuombea ububujiko huru wa Roho Mtakatatifu - ububujiko huru - udhihirisho mkubwa zaidi wa zawadi za Roho. Lakini zawadi za Roho hazipaswi kukoma kwa mikutano ya kanisa, kwa jumapili, kwa mikutano ya jumatano usiku au wakati wowote mnapokutana. Zawadi za Roho zinafaa kububujika katika maisha ya waumini. Kwa hivyo, ndio, ombea udhihirisho zaidi wa zawadi za Roho kwa kanisa, lakini ombea udhirisho mkubwa zaidi katika maisha yako. Hio ni sawa. Mungu anataka kukutumia katika zawadi za Roho. Inaanza kwa kuomba na kujifanya kupatikana kwa maombi. Juu ha hiyo, unaweza kusema, "Nimeona zawadi za ajabu za Roho. Kunaendelea vyema kanisani Jumapili au Jumatano." Nataka kukuhimiza leo: usiridhike na kile ulichokiona. Yesu alisema kuwa wale walio na njaa na kiu ya haki watashibishwa. Kwa hivyo usipokuwa na njaa, usipokuwa na kiu, hautaona zaidi. Kwa hivyo unapoombea udhihirisho mkubwa zaidi wa zawadi za Roho leo, inatupasa kutamani zaidi. Hio inamaanisha sisi ni wenye shukrani kwa yote tunayoyapitia lakini tunajua kwa sababu Mungu ni Mwenyezi Mungu – Ni Mungu Muweza yote – Yeye ni El Shaddai – ana zaidi kwa ajili yetu leo. Kwa hivyo nakuhimiza kuombea udhihirisho mkubwa zaidi wa zawadi za Roho kwa kanisa lako, kwa maisha yako binafsi, na kwa Mungu kwenda juu na zaidi ya kile ulichokiona hapo mbeleni. Kuwa na mchana mwema. Asante kwa kujumuika nasi kwa siku thelathini za maombi.

## PASTOR RONALD WALKER

Senior Pastor • Word of Faith
Virgin Islands

### Omba kwa ajili ya Familia na Ndoa zenye nguvu (Omba kutia nguvu familia ya nyuklia na kuwa Baba warudi nyumbani)

Habari. Jina langu ni Mchungaji Ronald Walker, kutoka Word of Faith, St. Thomas, Visiwa vya Virgin.

Leo katika maombi, tunataka kutilia mkazo kwa familia, na haswa kwa ndoa kwa sababu kama tunavyojua, kumekuwa na shambulio la kishetani dhidi ya kitengo cha familia na kile kinachoelezea maana ya familia.

Tazama, Neno la Mungu linasema katika Mwanzo sura ya pili, mstari wa ishirini na nne, “Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.” Hivi ndivyo Mungu anavyofafanua maana ya familia. Tunaona pia shambulio kubwa juu ya ndoa kwa ujumla. Tazama, adui anataka kuleta mgawanyiko wakati inapaswa kuwa ono moja. Anajua kulingana na Marko sura ya tatu, mtari wa ishirini na tano, “Na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama.”

Kwa hivyo ni muhimu kuwa tuuombee umoja wa familia. Kwa nini? Ili tuzione familia zilizo na umoja na nguvu bila kujali ni nini kinachowajia, bila kujali hali wanazoweza kukabiliana nazo.

Tunajua kinachotendeka wakati kila mmoja katika familia anatekeleza jukumu lake. Kama inavyosema katika Waefeso sura ya sita, mstari wa kwanza, “Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndio amri ya kwanza yenye ahadi;” Hili ndilo jukumu la watoto. Kisha inaongea kuhusu jukumu la baba katika mstari wa nne, “Nanyi, akina Baba, msiwachokoze watoto wenu: bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana.” Tazama, jukumu hili linapoathiriwa, huathiri nguvu ya familia ya nyuklia. Kwa hivyo tunaomba na kufanya dua, na kufanya maombezi kuwa baba wawe baba kama vile Mungu amewaagiza wawe na tunawaombea pia baba ambao hawajakuwepo katika maisha ya watoto warudi nyumbani tena.

Kisha tunaona jukumu la mama kwenye Mithali sura ya thelathini na moja mstari wa ishirini na saba. Tambua jukumu lake, “Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake, wala hali chakula cha uvivu.” Kwa sababu gani? Kwa sababu ya bidii yake ya kuitunza familia yake. Inaendelea kusema – nikisoma kutoka kwa Biblia iliyokuzwa, “Wana wake huamka na kumwita mbarikiwa (mwenye furaha, bahati nzuri, na kuonewa wivu); na mumewe huringa naye na kumsifu, [akisema], Binti za watu wengi wamefanya kwa wema, kwa heshima, na wema [kwa nguvu ya tabia iliyo thabiti katika wema], lakini wewe umewapita wote.” Tazama, wakati unayo familia nyuklia yenye nguvu, isiyotawanyika, mahali watoto wanaheshimu jukumu lao mbele ya Mungu na kuwekwa chini ya ulinzi wa wazazi wao - baba anaheshimu jukumu lake mbele ya Mungu - mama anaheshimu jukumu lake mbele ya Mungu - hiyo familia itaweza kusimama imara bila kujali ni nini kinachoweza kuwajia.

Kwa hivyo tunatazamia kuwa na familia za nyuklia zenye nguvu katika mwaka wa elfu mbili na ishirini na nne (2024). Tunatazamia kuwa na familia za nyuklia zisizotawanyika katika mwaka wa elfu mbili ishirini na nne. Tunatazamia kuwa na akina mama wema kwa nyumba zao katika mwaka wa elfu mbili ishirini na nne. Na tunatazamia baba wawe manyumbani mwao na wawe waume shujaa katika nyumba zao katika mwaka wa elfu mbili ishirini na nne.

Tunayo mengi ya kutazamia katika mwaka wa elfu mbili ishirini na nne panapohusu familia, kwa hivyo tumsifu Mungu kama wanaojua kuwa tayari imetendeka.

## MINISTER JASON MITCHELL

Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

### Ombea Tawi la Kutunga Sheria la Serikali

Karibu kwa siku ya kumi ya siku thelathini za kampeni yetu ya maombi. Jina langu ni Mtumishi Jason Mitchell na mimi ni mtumishi mfanyikazi hapa Southfield, Michigan. Leo tutaomba kwa ajili ya mabaraza yote mawili ya kongamano – hayo ni Bunge na Seneti. Popote ulipo duniani, unapaswa kuliombea bunge lako la kitaifa na Seneti.

Mtume Paulo hutuambia katika Timotheo wa kwanza sura ya pili, mstari wa kwanza hadi wa nne, "Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka wote waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli."Tunataka kuomba kuwa Mungu, Bwana wa Mavuno, awatume wafanyikazi katika tawi la kutunga sheria – mtu ambaye kutoka kwake watalisikia na kulipokea Neno la Mungu litakaloongewa ili wapate kuzaliwa upya.

Tunataka pia kuomba kuwa Mungu atawapa hekima walioko kwenye nafasi ya uongozi, wanapowaongoza wajumbe wa baraza zao. Tunataka pia kuomba kwa ajili ya wafanyikazi wa tabaka zingine. Tunataka kuomba kuwa Mungu awape hekima ili waweze kutekeleza ofisi waliochaguliwa kimaadili, kikatiba na kibiblia.

Tunataka zaidi kuomba kuwa Mungu awape kibali Wakristo- wanaume na wanawake wacha Mungu - kuzishika nyadhifa katika ofisi zao - kuwa wakurugenzi wao wa sheria, wasaidizi wao wa utawala, washauri wa kamati, na wakuu wao wa kazi. Tunataka pia tuombe kuwa ikiwa kunaye anayewashauri au kuwaongoza kuelekea uasi, kwamba watu hao waondolewe. Tunataka kuomba kuwa Roho Mtakatifu aliangukie Kongamano- kwamba aihudumie mioyo ya kila mwanachama – kuwa kila mswada, kila azimio litakalotoka kwa kamati liwe jambo litakalolielekeza taifa kwenye ucha Mungu, kuelekea njia ya Mungu ya kutenda na kuwa sawa.

Tunataka pia kuomba kuwa Mungu awape kibali wanaume na wanawake wacha Mungu wachaguliwe, wateuliwe katika nyadhifa hizi mbalimbali za ubunge ili taifa hili lielekezwe kwa njia za Mungu – njia yake ya kutenda na kuwa sawa. Sasa na tuombe.

**MINISTER KILA TURNER**
Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

## Ombea Mfumo wa Elimu

Hujambo na karibu tena kwa siku zetu thelathini za maombi. Leo tunaomba kuhusu mfumo wa elimu nchini mwetu. Haijalishi pale ulipo duniani, tunahitaji kuwaombea wale wote walio na jukumu la kuwasomesha watoto wetu katika chekechea na kitalu hadi vyuo vikuu vyetu na vyuo vya taasisi, na hata ngazi za uzamili. Katika shule zetu, wamehama kutoka kutoa habari na maagizo tu hadi mafundisho ya wazi ya mtazamo wa ulimwengu na tunaweza kukomesha hili, kwanza kabisa, kupitia kwa Roho kwa maombi. Kwa hivyo tunaenda kuomba haswa kulingana na Neno.

Bwana hutuambia kuwa tuwaombee walio mamlakani ili tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Na tunahitaji hivyo vitu vyote katika darasa zetu. Kwa hivyo leo muombee Katibu wako wa Elimu katika ngazi ya kitaifa pamaoja na ngazi la jimbo au baraza la uongozi – wale walio na wajibu wa kutengeneza sera ambazo zinaathiri mifumo ya shule zetu. Waombee kwa majina. Kwanza kabisa, kama hawajazaliwa upya tayari, omba kuwa wampokee Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Kisha, omba kuwa wajazwe na maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa rohoni. Omba kuwa wazungukwe na ushauri na washauri wa kimungu – wale ambao wanao moyo wa kumsikia Bwana na kuufuata mpango Wake.

Tunapaswa kuliombea jambo hilo kwa walimu wetu na wasimamizi wa shule zetu – kuwa watakuwa wazi na tayari kuupokea mwelekeo wa Bwana. Omba kwa ajili ya wale walio na ushawishi, kama wasanidi wa mtaala na vyama vya elimu. Wale wanayo sauti katika shule zetu – tunapaswa kuomba kuwa sauti yao inaidhihirisha roho ya Mungu. Tuwaombee wanafunzi wetu – kwamba ni wenye kasi ya utambuzi – ni wepesi wa kuelewa na ni wamakinifu – wenye wepesi wa ufahamu – kuwa macho ya mioyo yao yatiwe nuru ili walijue tumaini waliloitiwa.

Tunapaswa kuombea ulinzi juu ya shule zetu. Wafunike na damu ya Kristo ili silaha yoyote iliyotumwa kinyume chao isifaulu. Na mwishowe, tunafaa kuwaombea wazazi wetu – kuwa haki yao itarejeshwa na kuongezwa na kuwa watakuwa na sauti katika shule katika jina la Yesu.

**PASTOR JOEL JENKINS**
Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

## Waombee Vijana Wetu na Watoto Wetu

Habari na karibu kwa siku ya kumi na mbili. Leo tutawaombea vijana wetu na watoto. Unajua, ninakumbushwa wakati nilipokuwa mchanga. Tulikuwa na mazoezi ya kimbunga. Sasa, vijana wa leo hujizoesha kile ambacho kinaitwa mazoezi ya wapiga risasi. Vijana leo wanayo mambo mengi zaidi wanayoshughulika nayo ambayo hatukupata kushughulika nayo nilipokuwa mchanga. Kwa hivyo nafikiri ni muhimu kwetu kuwaombea vijana kuwa, kwanza, wajue kuwa wanapendwa. Biblia inaongea kuhusu pendo lililo kamili huitupa nje hofu. Kwa hivyo naamini kuwa ikiwa tutaomba wajue kuwa wanapendwa, hawapaswi kuwa waoga kuhusu kile siku inaweza kuleta. Pia naamini kuwa kwa vijana wetu twapaswa kuomba kwamba wajue wao ni kina nani na wito wao ni upi.

Katika Yeremia sura ya ishirini na tisa, inaongea kuhusu kuwa Mungu anayajua mawazo anayotuwazia sisi – Anajua mipango aliyo nayo kutuhusu na kutupa tumaini siku zetu za mwisho. Nafikiria kuwa ni muhimu tuwaombee vijana wetu kwamba wajue wao ni kina nani na waujue wito wao.

Kwa hivyo leo, unapojitayarisha kuomba, hakikisha kuwa unaomba kuwa vijana wetu wapate kujua wanapendwa, wapate kujua wameitwa kufanya nini, na wapate kujua wito wao ili wawe kila kitu Mungu alichowaita kuwa.

## PASTOR GREGORY DONALDSON

Keith Butler Ministries
Cork, Ireland

### Omba kuwa Neno la Mungu lienee kotekote Duniani

Karibu kwenye siku thelathini za maombi. Jina langu ni Mchungaji Gregory Donaldson. Kiini cha maombi ya leo ni kuwa Neno la Mungu lienee kotekote duniani. Neno lienee inamaanisha kusonga au eneo lilofunikwa na jambo fulani. Tutaomba leo kuwa Neno la Mungu litasonga au kuenea eneo lote la kile tunachoita dunia, ulimwengu.

Maandiko yanatuambia katika Wathesalonike wa pili sura ya tatu, mstari wa kwanza, "Hatimaye, ndugu, tuombeeni sisi," Inatwambia papo hapo katika andiko – hilo neno 'sisi' linamaanisha sisi, wewe na mimi. "ili ujumbe wa Bwana uzidi kuenea upesi na kupokelewa kwa heshima kama vile ulivyo kati yenu:" Kwa hivyo tunaomba leo kuwa Neno la Mungu liende kila mahali duniani na pia liinuliwe na kusifiwa na kutukuzwa, kama vile mimi na wewe hufanya. Siombi tu kuwa lienee, lakini tunaomba kuwa watu walipokee, walikumbatie na waliinue na kulitukuza Jina Lake. Hilo linafanyikaje? Ni kama uvumi. Uvumi huenea kwa sababu watu huusikia na huongea kuuhusu. Tutaombeana mmoja kwa mwingine na kuombea majirani na marafiki na familia na wapendwa kuwa walishiriki Neno la Mungu tunavyoshiriki nao Neno la Mungu kwa mchakato huo lienee kama uvumi kote duniani.

Tutaombea makanisa na viongozi wa kanisa na makutano. Tutaombea ujasiri ili waende maeneo na wafanye mambo yale Mungu amewaita kufanya. Tutaombea tekinolojia na kampuni. Tutaombea satelaiti na tuombe kwa ajili ya tovuti na tutaomba kwa ajili ya uvumbuzi wote wa busara wa kimungu Anaoweza kuutumia ili kulieneza Neno la Mungu kotekote duniani.

Lakini kwanza kabisa na kubwa zaidi, tutaombea utiifu. Tutaomba kuwa sote tuwe watiifu wa wito wa Mungu kwa maisha yetu. Na kwa wale wote ambao hawajaokoka, tutaomba kuwa wafanyikazi wapite njia zao ili wapate kuokoka na kulishiriki Neno la Mungu, pia.

Kwa hivyo nawauliza, kuwa muuinganishe imani yenu kwa yangu, tunapoomba siku nzima kuwa Neno la Mungu lienee duniani kote na inaanza na mimi na wewe.

Mungu akubariki. Roho wa Mungu yupo juu yako. Tuombe.

# PASTOR DERRICK GREENE

Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

## Ombea Utume na KBM (Omba kuwa Mungu afungue milango kwa mataifa)

Habari.  Jina langu ni Derrick Dwayne Greene, mmoja wa wachungaji wafanyikazi hapa katika kanisa la Word of Faith International Christian Center. Karibu kwenye siku ya kumi na nne ya siku zetu thelathini za kampeni ya maombi. Mada yetu ni kuombea utume na KBM, kuwa milango ya Mungu itafunguka ili twende mataifa yote.

Ninataka kuanza na kitabu cha Matendo ya Mitume ambacho kinaongea kuwa tutapokea nguvu wakati Roho Mtakatifu atawashukieni, ambayo tumeipokea tayari. Na inasema kuwa sisi tuwe mashahidi au wanavita wa maombi au wafanyikazi Yerusalemu, Yudea, Samaria, na hata mwisho wa dunia. Na cha msingi, hicho ndicho KBM inachokifanya na ndicho sisi kuwa wanavita wa maombi – tunachojumuika kuwaweka kwenye hali ya kuinuliwa ili tuipeleke Injili kotekote duniani.

Ni wazi kabisa kuwa Yesu alituokoa kwa kusudi, sio tu la kuomba, lakini kuifanya kazi. Basi tujishughulishe na mambo ya Mungu.

Katika Luka sura ya kumi, mstari wa pili – ni mstari wa kuvutia sana na unasema hivi, "mwombeni mwenye shamba, atume wavunaji shambani mwake." Vizuri. Bila shaka, mavuno ni dunia – bara zote saba. Na KBM na maombi yetu yatayafunika ili tuendelee kuyaleta mabadiliko makubwa duniani kupitia kwa maombi katika Ufalme wa Mungu. Bila shaka, katika Ufunuo sura ya tatu – neno la muhimu sana pia ambapo Yesu anaongea kuhusu kuifungua milango ambayo hakuna awezaye kuifunga- kuifunga milango ambayo hakuna awezaye kuifungua.

Jukumu letu, kupitia maombi, ni kulitayarisha jukwaa –kukiweka kiwango - kuwa wale ambao huweka anga la milango kufunguka popote Bwana anapoituma huduma hii. Ni fursa na heshima yetu kuwa mara nyinyi hatuwezi kwenda binafsi lakini tunaweza kuiunga mkono kupitia kwa maombi yetu na kwa utoaji wetu – kupanda kwa KBM ili kazi ifanyike bila pingamizi, bila ukosefu, bila usumbufu wowote.

Neno la Mungu ni wazi sana na tunapojiunga wenyewe pamoja kwa maombi, tunafanya litendeke. Basi tuonane kesho kwa siku yetu nyingine ya maombi. Mungu akubariki na tunakupenda.

## PASTOR TIMOTHY RAMSAY

Senior Pastor • The Place of Grace UK
London, England

### Ombea Wakristo wawe na Athari Kubwa Zaidi katika Sekta ya Burudani (Runinga, Filamu, Muziki, Ukumbi…)

Karibu kwenye siku ya kumi na tano ya siku thelathini za kampeni yetu ya maombi. Jina langu ni Timothy Ramsay. Mimi ni Mchungaji Mkuu katika The Place of Grace- London, Uingereza. Leo tutaombea Wakristo wawe na athari kubwa zaidi katika sekta ya burudani.

Katika Waefeso sura ya nne, mstari wa ishirini na saba tumeambiwa tusimpe ibilisi nafasi. Neno hilo 'nafasi' tunavyolichambua kwa Kigiriki kihalisi linamaanisha ardhi au eneo. Kwa hivyo kile Paulo anachotuambia ni kuwa hakuna mahali, naamini, duniani ambapo Mungu ameumba ambapo waumini wanapaswa kuamini ili shetani azidi kutawala.

Kwa kweli, tumeambiwa na Yesu katika vitabu vya injili kuwa tunapaswa kufanya biashara hadi atakapokuja. Hivyo kuna eneo la ushiriki wa namna fulani. Naamini, kama wakristo, tunamwacha shetani huru akimbie na kufanya mambo yake, haswa kwa sekta ya burudani, iwe kwa muziki, iwe kwa ukumbi au sinema, au iwe kwa sanaa. Lakini naamini kuwa tukiomba, Mungu atawainua wake na waume walio na wito tofauti kwenye sekta hio ambao watatumika sana na Mungu kuileta Injili yake, kuuleta uhai wake katika eneo ambalo kwa kweli lina giza.

Jambo mojawapo kuhusu sekta ya burudani ni pia kuwa huwa na ushawishi mkubwa na athari. Hii ndio sababu, sisi kama waumini, hatuwezi kuiacha peke yake. Inabidi tuingie huko. Inabidi tuanze kuandika, kuigiza, kuimba, kujenga mambo yetu wenyewe yatakayoathiri kizazi hiki na mbali zaidi, kama tulivyoona sekta ya burudani ilivyowaathiri watu hapo zamani. Kwa hivyo hapa sio mahali ambapo tutamruhusu shetani kuwa na utawala huru.

Naamini kuwa Yesu anataka kufanya athari huko Hollywood. Anataka kufanya athari Nollywood na Bollywood na katika vituo vyote vya burudani vya mataifa. Anataka kufanya athari ili Jina Lake liinuliwe juu na awavute watu wengi zaidi kwake. Kwa hiyo tuombe. Hatutampatia shetani nafasi, katika jina kuu la Yesu.

**PASTOR JOHN WARD**
Word of Faith Int'l Christian Ceter
Southfield, Michigan

## Ombea Tawi la Mahakama la Serikali

Tumsifu Bwana kila mmoja. Karibu kwenye siku ya kumi na sita. Leo tunaliombea tawi la mahakama la serikali. Hebu tuangalie Injili ya Mtakatifu Luka sura ya kumi na nane, kuanzia mstari wa kwanza. Na inasoma hivi, "Akawaambia mfano ya kwamba, imewapasa kumwomba Mungu sikuzote, wala wasikate tamaa; akasema, Palikuwa na kadhi katika mji fulani, hamchi Mungu, wala hajali watu. Na katika mji huo palikuwa na mwanamke mjane, aliyekuwa akimwendea-endea, akisema, nipatie haki na adui wangu. Naye kwa muda alikataa; halafu akasema moyoni mwake, ijapokuwa simchi Mungu wala sijali watu, lakini, kwa kuwa mjane huyu ananiudhi, nitampatia haki yake, asije akanichosha kwa kunijia daima. Bwana akasema, sikilizeni asemavyo yule kadhi dhalimu."

Hivyo hapa Yesu anaongea kuhusu maombi. Hilo ni kweli tegemezi. Lakini pia anatumia mfano wa kadhi dhalimu na Maandiko yanaendelea kutuambia kuwa alilipata jibu la maombi yake kwa sababu hakukoma kuomba. Na Mungu anataka tuwaombee mahakimu. Ni mapenzi ya Mungu kuwa mahakimu wako katika nafasi ya moyo Wake Mwenyewe. Na tunajua ya kwamba kutoka Timotheo wa kwanza sura ya pili kuwa tunafaa kuwaombea watu wote na sanasana wale walio mamlakani ili tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Kwa hivyo inahitaji maombi.

Isaya sura ya kwanza, mstari wa ishirini na sita inatwambia hivi, "Nami nitarejeza upya waamuzi wako kama walivyokuwa hapo kwanza," Mungu anawataka waamuzi wanaoupendeza moyo wake mwenyewe. Anawataka waamuzi watakaofanya uamuzi wa haki. Na inatupasa kuwaombea waamuzi. Inatupasa tuwaombee watende kazi katika hali ya kumcha Mungu ili wahukumu kwa hukumu la haki.

Yohana saba mstari wa ishirini na nne inasema hivi, "Basi msihukumu hukumu ya macho tu, bali ifanyeni hukumu iliyo ya haki." Hapa Marekani – Najua kuna watu kutoka kila mahali duniani – huombea majaji wa mahakama kuu nao ni Hakimu mkuu Roberts, Hakimu Thomas, Hakimu Alito, Hakimu Sotomayor, Hakimu Kagan, Hakimu Gorsuch, Hakimu Kavanaugh, Hakimu Barrett na Hakimu Jackson. Hawa ndio majaji na tunawaombea. Mahali popote ulipo, pia nawe unafaa kuwaombea hakimu wako. Kuwa na siku njema sana.

## PASTOR GEORGE RIGOS

Senior Pastor • Kentro Pistis
Athens, Greece

### Waombee Wakristo Wanaoteswa

Habari. Mimi ni mchungaji George Rigos kutoka Athene, Greece. Mimi ni mkurugenzi wa KBM Ulaya na mchungaji wa kanisa letu hapa. Ni vyema sana kuwa nawe leo katika siku hizi thelathini za maombi. Tayari tuko kwenye siku ya kumi na saba. Lo. Ajabu. Unajua kuwa maombi yanafanya kazi na maombi yetu yanaleta mabadiliko.

Leo tutawaombea Wakristo wanaoteswa. Hili ni jambo ambalo ni halisi. Sio tu kutoka nyakati za Biblia, kutoka nyakati za Paulo, lakini ni jambo ambalo ni halisi sana. Bado linatendeka leo kote duniani. Katika kusanyiko letu, tunao wakimbizi kutoka Iran ambao hawawezi kurudi kwao kwa sababu familia zao zitawaua ikiwa watarudi. Na tuko nao kutoka mahali kwingine. Ninaye rafiki kutoka Uturuki. Alimkubali Yesu na alifurahishwa mno na hili. Babake alipogundua alituma muuaji kujaribu kumuua. Leo yuko na alama kwenye shavu lake kwa sababu mtu huyo alikuja nyuma yake kumuua. Alimkosa, Mungu asifiwe. Lakini alipata shavu lake. Na bwanake alifungwa jela kwa kuamini.

Ni halisi. Ni ukweli. Mateso yanafanyika, lakini hata Marekani na katika mataifa yetu ya ulimwengu wa kwanza na mataifa ya magharibi. Kunayo mateso haya kwa sababu hakuna anayetaka Neno la Mungu, hakuna anayeutaka ukweli. Wanataka kuifuata giza hiyo inayodaiwa na kusukumwa hivi sasa. Kwa hivyo tunahitaji maombi kwa sababu kuna mateso ambayo ni ya kimwili, kunayo mateso ambayo ni ya Kiroho, kunayo mateso, kwa kila ulimwengu. Tukiangalia Waefeso sura ya sita, mstari wa kumi na nane inasema, “Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;” Inatupasa kuuombea Mwili wa Kristo kote duniani. “Pia na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya injili, Ambayo kwa ajili yake mimi ni mjumbe katika minyororo: hata nipate ujasiri katika huyo kunena jinsi inipasavyo kunena.” Kwa sababu hatutaki mateso haya yatuachishe kushiriki. Hilo ni ombi la maana unapoomba leo – kuwa tuendelee kuwa jasiri, bila kujali kinachokuja dhidi yetu, bila kujali kinachojaribu kutuachisha- kuwa tutaendelea kuwa jasiri katika kushiriki Neno na kufanya watu wajue kuwa Yesu yu kweli na kuna suluhisho lao – kwa sababu mimi na wewe, ndugu na dada yangu, ndio suluhisho la ulimwengu huu unaoumia.

Katika Waebrania kumi na tatu, tukiangalia mstari wa kwanza, inasema, “Upendano wa ndugu na udumu. Msisahau kuwafadhili wageni: maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua.” Usijifungie nje. Usifunge dunia kwa sababu wanakuja dhidi yetu. Hapana. Tunaendelea kuwa jasiri. Tunaendelea kuwa na nguvu. Tunaendelea kulitangaza Neno. Na inasema kuwakumbuka wafungwa ambao wamefungwa pamoja nao – wale ambao wanadhulumiwa– kwa kuwa wewe mwenyewe uko katika mwili pia. Kunao wafungwa wanaofungwa kwa sababu ya imani yao. Inatupasa kuwaombea. Inatupasa tuwe tukiombea kila mtu. Inatupasa tuwe tukiliombea kanisa, katika siku hizi na nyakati, kuwa tuwe jasiri na tuendelee kuwa nuru ya dunia. Mungu akubariki leo unapoomba. Usikate tamaa.

## PASTOR FRANK DAVIS

Campus Pastor • Faith4Life
Toledo, Ohio

### Ombea Kanisa Lako

Habari. Karibu kwenye siku thelathini za maombi. Natumai kuwa unafurahia sana wakati huu wa maombi. Leo tutaliombea kanisa letu na washirika wake. Haijalishi wewe huenda kanisa gani. Ni muhimu kwetu kuliombea kanisa na watu katika kanisa.

Katika Zaburi mia moja thelathini na tatu, mstari wa kwanza, Daudi anatuambia jinsi ilivyo vyema na vizuri ndugu kuishi pamoja. Na katika mstari wa tatu, anaendelea kusema, “hapo Mungu aliamrisha baraka.” Anaposema ‘hapo,’ anaongea kuhusu nini? Anaongea kuhusu ndani ya mahali tunapoishi kwa umoja. Mahali hapo, Mungu huamrisha baraka. Kwa hivyo leo tunapoomba, tunataka kuhakikisha kuwa tumeombea makanisa yetu na kila mtu katika makanisa yetu waishi pamoja kwa umoja.

Tunataka kuomba kuwa kila mmoja atembee kwa upendo na pia tunataka kuomba dhidi ya ugomvi wowote kanisani kwa njia yoyote, umbo, fomu au mtindo. Omba kuwa tuishi pamoja kwa umoja.

**PASTOR FRANK AMOAKO**
Senior Pastor • Word of Life
Brussels, Belgium

## Ombea Amani ya Yerusalemu

Habari familia. Karibuni kwenye siku ya kumi na tisa ya kampeni hii nzuri ya maombi. Leo tunaombea Yerusalemu. Tunaombea amani ya Yerusalemu kulingana na Zaburi mia moja ishirini na mbili, mstari wa sita na inasema hivi, "Utakieni Yerusalemu amani: na wafanikiwe wakupendao."

Bila shaka, neno la Kiebrania la amani ni shalom. Linamaanisha ustawi; linamaanisha pumziko; linamaanisha afya; linamaanisha mafanikio; pia linamaanisha usalama. Kwa hivyo tumeitwa kuombea usalama wao na ustawi wao na ustawi wa Yerusalemu. Tunajua kuwa Yerusalemu ni moyo wa Mungu. Ni mji wake mtakatifu. Ni mahali maarufu sana – mahali pa kihistoria – na iko na mahali kwa unabii wa Biblia siku zijazo. Kwa hivyo leo, tufanye kulingana na maandiko. Tuombe kama Mungu anavyotaka tuombee amani na ustawi wa Yerusalemu. Pia tambua kuwa ilisema, "na wafanikiwe wakupendao." Kwa hivyo kuna kufanikiwa ambako huja kwa kuombea na kuupenda mji wa Yerusalemu. Mungu akubariki na uwe na siku njema.

## PASTOR MARIO BENNETT

Senior Pastor • Faith4Life
Round Rock, Texas

### Ombea Kusudi lako na Mahali pako pa Kazi

Karibu kwenye siku ya ishirini ya maombi. Tumeendelea vyema sana. Nimeifurahia kabisa. Najua pia nawe vilevile umefurahia. Tuna siku kumi zaidi zilizobakia. Kwa hivyo nataka kukuhimiza- tumalize kwa nguvu kwa sababu maombi yetu hubadilisha dunia.

Leo tutaongea kuhusu kusudi lako na mahali pako pa kazi. Kila wakati napenda kuanza na Bwana Yesu kwa sababu yeye ndiye mfano wetu. Nataka kushiriki nawe vipande vitatu vya Maandiko. Katika Yohana wa kwanza Sura ya tatu, inasema kwamba kwa kusudi hili, Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azifunje kazi za ibilisi. Pia nataka kuwaambia kuwa Yesu alisema mwenyewe, "Imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu." Na la tatu, katika Matendo sura ya kumi, mstari wa thelathini na nane – najua unajua huu, "jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye."

Nataka utambue kuwa kuna mambo matatu yaliyotendeka. Yesu alikuwa na kusudi. Alielewa kuwa lazima awe kwenye kazi ya kulikamilisha kusudi lake na Mungu alimneemesha kwa kusudi lake. Sawia, mimi nawe tumeneemeshwa kwa kusudi. Inatuambia katika Wakorintho wa kwanza sura ya kumi na mbili, "Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka." Je wajua kuwa mkono na goti yote yana kusudi tofauti? Mkono unapofanya kazi yake, basi mwili wote unakuwa bora. Lakini endapo mkono hautafanya kazi yake, mwili wote unaumia. Ndivyo ilivyo mimi nawe tusipotembea katika kusudi letu.

Kwa hivyo Mungu amesema nini kuhusu kulikamilisha kusudi letu? Na tuangalie Wakolosai sura ya tatu na inasema kwenye mstari wa ishirini na mbili, "Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote, si kwa utumwa wa macho, kama wajipendekezao kwa wanadamu, bali kwa unyofu wa moyo, mkimcha Bwana. Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu, mkijua ya kuwa mtapokea kwa Bwana ujira wa urithi." Nataka kushiriki hili nawe: Mungu ametuita kumfanyia kazi na sio kumfanyia mwingine yeyote. Wakati inaposema tufanye kazi kwa moyo wote kwa Bwana, inasema, "Kwa moyo wako wote fanya kile ulichoitwa kukifanya, ukitambua kwamba Baba yako hukuona na atakuzawadi."

Jambo lingine ninalotaka kushiriki nawe linalozungumziwa katika Zaburi sura ya kwanza ni kuwa kama waumini, tunapofanya kile Mungu alichotuita kukifanya, kuwa itatusababisha kufanikiwa kwa chochote tukifanyacho. Kwa hivyo nataka kukuhimiza leo - tuyafanye mambo matatu. La kwanza, tuombe ili tulijue kusudi letu. La pili, tuombe kuwa tuingie kwa kusudi hilo. Na la tatu, tuombe kuhusu mahali petu pa kazi, ili kusiwe na ugomvi, hakutakuwepo utawanyikaji. Lakini tuombe kuwa kuwe na amani, tuombe kuwe na maelewano, na tuwaombee walio kwenye mamlaka kwa sababu ni kupitia kwa Mungu ambapo tunaweza kufanya yote. Na tuombe.

## PASTOR REGINALD WALKER

Senior Pastor • Word of Faith Christian Center
Vicksburg, Mississippi

### Tuwaombee Raia Wetu Waandamizi

Salamu kwa kila mmoja na karibu kwa siku ya ishirini na moja ya siku zetu thelathini za maombi. Mimi ni Reginald Walker, Mchungaji Mkuu wa Word of Faith Christian Center, Vicksburg, Mississippi na kazi yangu ya kampeni ya mwaka huu – mimi mwenyewe nikiwa miaka sitini na tano – ni kutuombea sisi waandamizi.

Sehemu ya pili katika Wakorintho wa Pili sura ya nne, mstari wa kumi na sita katika Toleo lililokuzwa inasoma, "ingawa mtu wetu wa nje [anaendelea] kuharibika na kuwa dhaifu, bado mtu wetu wa ndani anakuwa [anaendelea] upya siku baada ya siku." Ndio, mwili wetu unavyoangamia na kuzeeka kunaweza kuleta baadhi ya maumivu na uchungu, lakini mtu wako wa kiroho anaweza kufanywa upya kila siku. Tuombe kuwa kila raia mwandamizi atagundua kuwa bila kujali sehemu yao, ikiwa bado unapumua Mungu yuko na kusudi lako. Mtafute kwa hilo. Zaburi sabini na moja mstari wa kumi na nane kutoka kwa Biblia iliyokuzwa inasoma, "Naam, na hata nikiwa ni mzee mwenye mvi, ee Mungu, usiniache, [lakini niweke hai] hata nitakapowaelezea watu wa kizazi [hiki] nguvu zako, na kila atakayekuja uweza na nguvu zako."

Imesemekana kuwa uzoefu ndio mwalimu mzuri zaidi. Sikubaliani. Uzoefu wa watu wengine ndio mwalimu mzuri zaidi na ukishiriki uzoefu wako unaweza kuusaidia uzao mchanga ili kuyazuia makosa mengi. Hekima ni kitu ambacho hakiwezi kununuliwa lakini kinaweza kushirikiwa. Shiriki hekima yako.

Isaya arobaini na sita, mstari wa nne, ikitoka kwenya Bibilia iliyokuzwa, inasema, "Na hata uzee wenu mimi ndiye, na hata wakati wenu wa mvi nitawachukueni. Nimefanya, nami nitachukua; naam, nitachukua na kukuokoa." Kwa maneno mengine, bila kujali umri wako, Mungu yu nawe. Kwa wale wetu ambao wako sawa, huu sio wakati wa kukata tamaa. Tupo kwenye robo ya nne. Abrahamu alikuwa na miaka sabini na tano Mungu alipomuita kutoka Haran. Musa alikuwa na miaka themanini alipowaongoza wana wa Israeli kutoka Misri na Kaleb alikuwa na miaka themanini na tano alipomuambia Yoshua ampe mlima wake akisema, "Mimi nina nguvu zangu hivi leo kama nilivyokuwa siku hiyo Musa aliyonituma."

Kuwa mzee ni baraka na ni heshima ambayo sio kila mtu anayepata fursa kufika uzeeni na kwa sababu Mungu amenipa nafasi hii, sitazamii kustaafu. Natazamia kuwa na moto zaidi. Tupo sasa kwenye siku kumi za mwisho za kampeni hii na himizo langu kwako ni kuwa umalize kwa nguvu. Na ombi langu kwa waandamizi wenzangu ni kuwa tufanye vivyo hivyo.

## PASTOR DON MANCHA

Senior Pastor • Faith Christian Center
San Francisco, California

### Ombea Wanaopambana na Uraibu na Masuala ya Afya ya Akili

Bwana asifiwe. Habari ya Asubuhi. Hii ni siku ya ishirini na mbili ya siku zetu thelathini za maombi na mimi ni Mchungaji Don. Asubuhi hii tutawaombea watu wanaopambana na uraibu au masuala ya Afya ya Akili.

Ni muhimu sana kuwa tuwaombee watu na tuwaombee kulingana na Neno la Mungu, ambalo ni mapenzi ya Mungu. Kwa hivyo tuangalie Timotheo wa kwanza sura ya pili, mstari wa nne na Neno linasema, "Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli." Hayo ndiyo mapenzi ya Mungu kuwa watu wote waokolewe. Sasa, neno hilo waokolewe kwa Kigiriki – sozo – humaanisha kukombolewa, kufanywa mzima, kuhifadhiwa, salama kutokana na hatari, hasara au uharibifu. Hayo ni mapenzi ya Mungu. Haijalishi ni aina gani ya hali unayopitia – marafiki zako au familia yako au mnaofanya nao kazi – haijalishi wanachokipitia, ni mapenzi ya Mungu kuwa waokolewe. Kwa hivyo waombee hivyo kwa mamlaka yake Yesu. Pia unapoombea familia yako au mnaofanya nao kazi au wengine wanaopambana na hali hizi, ombea hekima: cha kufanya, cha kusema, namna ya kukisema, wakati wa kukisema, mtazamo utakaousema nao.

Enda kwenye Waefeso sura ya sita, mstari wa kwanza. Anaongea kuhusu wazazi kuhusiana na wanafamilia wao, haswa watoto wao. Lakini hapa tuuangalie mstari wa nne, "Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana." Hivyo unaposhughulika na watoto wako, hata kama unayo mamlaka, hata kama unaifanya kazi kwa niaba yao, yachague maneno yako kwa hekima. Tusome hii kutoka Toleo la New Living – Waefeso sura ya nne, mstari wa sita, "Akina baba, [c] msiwachokoze watoto wenu kwenye hasira kwa jinsi mnavyowatendea. Bali, waleeni na nidhamu na maelekezo yanayotoka kwa Bwana."

Omba kuwa Bwana akupe maneno ya kusema na jinsi ya kuyasema na wakati wa kuyasema wakati unaposhughulika na wanafamilia na marafiki wanaoteseka kutokana na uraibu na masuala ya afya ya akili. Omba Mungu hekima Naye atakupa. Barikiwa.

**MINISTER LINDA BURDETTE**
Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

## Ombea Uchaguzi wa Viongozi Wanaomcha Mungu

Habari. Jina langu ni Linda Burdette na leo ombi letu linalenga kuwaombea viongozi wanaomcha Mungu. Leo tutalenga uongozi wa Taifa letu. Bibilia hutuambia kuwa tunafaa kuwaombea walio na mamlaka juu yetu. Kwa kweli katika Timotheo wa kwanza sura ya pili, mstari wa pili unasema kwamba, "Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu." Hivyo Mungu anataka tuombe. Hilo ndilo jambo la kwanza ninalotaka ulijue.

Kwa nini anataka tuombe? Anataka tuombe ili tuwe na maisha ya utulivu na amani. Sasa maisha hayo ya amani na utulivu yanategemea baadhi ya mambo. Moja, inategemea ukweli kwamba tunahitaji kuomba. Sisi ni kina nani? Waumini. Kila muumini anapaswa kuutoa msaada wa Roho na kuomba.

Jambo la pili ambalo hayo maisha ya utulivu na amani yanategemea ni kuwa tuombe Mungu atupe viongozi wanaomcha. Sasa Mithali sura ya ishirini na tisa, mstari wa pili inasema hivi, "Wenye haki wakiwa na amri, watu hufurahi; bali mwovu atawalapo, watu huugua." Tunataka watu wa nchi zetu wafurahi. Kwa hivyo ukikubaliana nami kuhusu hilo, basi nataka uombe nami leo.

Tunataka kuomba kuhusu mambo fulani kuhusu serikali yetu. Tunataka kuomba kuwa Mungu atatupa viongozi wanaomcha – waume na wake wa Mungu wanaomwogopa – waume na wake wa Mungu wanaomtii – waume na wake wa Mungu waliojazwa na Roho Mtakatifu na wanaomruhusu Roho Mtakatifu kuwaongoza kwa mambo yote. Wakati unapoomba kuhusu mambo haya leo, utakapomalizia lugha yako ya maombi katika lugha yako asili, nataka ujikabidhi kwa Roho Mtakatifu na uombe zaidi katika Roho kwa sababu tunataka kuomba mapenzi kamili ya Mungu.

Nataka kukushukuru kwa kuungana nasi leo katika ibada yetu na tuombe Bibilia inavyotuelekeza kuombea viongozi wanaomcha Mungu. Mungu akubariki.

## PASTOR DEBORAH BUTLER

First Lady • Word of Faith Int'l Chrisitan Cebter
Southfield, Michigan

### Omba kuhusu Ulinzi wa Kimungu

Habari. Leo nataka kuongea nawe kuhusu ulinzi wa kimungu. Na Maandiko ambayo nitashughulika nayo ni Zaburi arobaini na sita inayosema, "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari;" Hakuna kitakachotuondoa kwa ukweli kuwa Mungu ndiye kimbilio letu na nguvu yetu. Kisha, katika Zaburi tisini na moja, ambayo ni mojawapo ya Maandiko ninayopenda zaidi kuhusu ulinzi wa kimungu, "Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu atakaa katika uvuli wake Mwenyezi. Nitasema, Bwana ndiye kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu nitakayemtumaini." Kwa hivyo kile ambacho nilitaka kukuambia – kwa kweli haya Maandiko wawili yanaenda sambamba. Alisema, "Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu…" Kwa hivyo mstari huu wa kwanza unavyo vipande viwili: moja ni sharti; moja ni ahadi. Sharti ni yule aketiye mahali pa siri pake Aliye juu. Aketiye inamaanisha kuishi ndani, kukaa ndani- kuishi, aishiye kwa Neno la Mungu. Kwa hivyo inamaanisha inakupasa kujua Neno la Mungu linachosema kuhusu ulinzi. Kuna mambo mengi yanayokuja na hilo. Haujiweki kwa njia ya taabu kimaksudi. Unamsikiliza Mungu kujua ni lipi unalofaa kulifanya na ni lipi usilofaa kulifanya kwa sababu unaishi katika Neno na unashiriki na Mungu kila siku. Unaongea na Roho Mtakatifu kila siku. Kila siku unamruhusu akuongoze na aziongoze hatua zako.

Kwa hiyo, hilo ndilo sharti kuwa unaketi mahali pa siri pake Aliye juu. Sasa hiyo ndio sehemu ya pili ya sharti. Lazima umtambue Mungu kama Mungu Mkuu zaidi. Yuko juu kuliko kila kitu. Kila Kitu hutegemea anachosema– tosha. Na hauelezei au kumuacha yeyote aielezee.

Sasa ahadi- atakaa kwenye uvuli Wake Mwenyezi. Kwa hivyo hilo ndilo ninalotaka ulikumbuke. Ni sawa kukaa. Na kuhusu ulinzi wa kimungu, lazima utimize sharti. Mungu akubariki.

## EVANGELIST KATHRYN STRAMLER

Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

### Omba Kuhusu Jeshi na Wahudumu wa Kwanza

Habari. Jina langu ni Muinjilisti Kate Stramler na leo ni siku yetu ya ishirini na tano ya maombi. Na leo tutaomba kuhusu jeshi, Wahudumu wa Kwanza, Wakuu wa Wafanyikazi na Idara ya Ulinzi.

Maombi, kama unavyojua, sio pendekezo bali ni amri. Inasema katika Timotheo wa kwanza sura ya pili, mstari wa kwanza hadi wa nne, "Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli." Tambua kuwa hakusema, "Ukitaka." Ni amri, sio pendekezo.

Katika Warumi sura ya kumi na tatu, mstari wa kwanza, anasema, "Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo umeamriwa na Mungu." Kwa hivyo hilo linakwambia nini? Linasema kuwa kila kitu huko Capitol Hill, kila nafasi, kila mtu anayehusika na kushughulika na mamlaka ameamriwa na Mungu. Haikusema kuwa unafaa kupenda kile unachofanya, lakini tunapaswa kuwaombea. Kwa hivyo kile tutakachokifanya ni kuwa tutaomba kuhusu ulinzi wa migawanyiko hii. Kwa hivyo tutaomba kwa ajili ya Ulinzi wa Jeshi, Mkuu wa Majeshi na Idara ya Ulinzi. Hilo ni la kwanza. Kwa hivyo tutaomba kuwa hakuna madhara au hatari itakayowajia wanapotumikia kwa niaba yetu.

La pili tutaomba kuhusu hekima ya Mungu na fikira za Kristo, na maamuzi yao yote yanayofanywa kuwa wasisikilize kushoto au kulia, lakini kwamba wafuate kabisa mapenzi ya Mungu kwa kila wafanyalo.

La tatu, tutaomba kuhusu mtazamo wa kimungu ili wafanye kinachohitajika kufanywa kwa kila hali watakayopatana nayo. La nne, Tutaomba kwamba Mungu awatume wafanyikazi wa kiroho kwenye njia zao ambao watawahudumia kwa njia ambayo wataipokea.

Kwa hivyo njoo. Tusichoke kutenda wema kwa sababu tunajua kuwa tu wanyonge tusipozimia roho. Hii ni biashara ya kifalme. Kwa hivyo tuombe.

## PASTOR EDWARD TAYLOR

Senior Pastor • Word of Faith Christian Center
Yazoo City, Mississippi

### Ombea Wale ambao Hawajaokoka na kuwa Wana Wapotevu Warejee

Karibu kwa siku ya ishirini na sita ya siku thelathini za maombi. Jina langu ni Mchungaji Edward Taylor na mimi ni Mchungaji wa Word of Faith Christian Center papa hapa Yazoo city, Mississippi.

Kazi yetu leo ni kuomba kwa ajili ya wale ambao hawajaokoka na pia tuwaombee wapotevu, kwamba wapate kurudi. Tunamtumikia Mungu wa rehema. Na kulingana na Neno linalopatikana katika Timotheo wa kwanza sura ya pili, na mstari wa nne, na pia katika Petero wa pili, sura ya tatu mstari wa tisa, ni mapenzi ya Mungu kuwa yeyote asipotee na kuwa wote wataokolewa. Kwa hivyo nakuuliza – tafadhali jiunge nami leo na tumuulize Mungu awatume wafanyikazi kwenye shamba. Tutembee kwa makubaliano kuwa hakuna atakayepotea na wote wataokolewa na wapotevu wote watarudi kwa Mungu. Je, uko tayari? Tuombe.

# PASTOR ANJOLO FIELDER

Campus Pastor • Faith4Life
Pensacola, Florida

## Omba kuhusu Nafasi za Kuwahubiria Wengine

Mkoje familia ya imani? Huyu ni Mchungaji Anjolo Fielder, Mchungaji katika kanisa la Faith4Life Pensacola, Florida. Karibu kwenye siku ya ishirini na saba ya siku zetu thelathini za maombi. Usirudi nyuma sasa. Endelea hata zaidi. Lengo letu leo la kuomba kwa ajili ya nafasi ya kuwahubiria wengine. Biblia hutuambia katika Petero wa kwanza, sura ya tatu, mstari wa kumi na tano, "Bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu, mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."

Kumbuka kile ambacho Mungu amekufanyia na ujue kuwa sio mapenzi ya Mungu kuwa mwema kwako tu na kwa maisha yako. Bali anataka kuwa hivyo katika maisha ya kila mtu. Leo tunaamini kuwa tutapata nafasi na kibali, milango itafunguka kwetu tuwekwe mbele ya wasioamini, iwe ni wanafamilia, mmoja kazini mwako, mmoja shuleni mwako, hata mmoja dukani. Na njia za hewa zitakuwa sawa kwetu ili kuanzisha mazungumzo na kushiriki Yesu nao.

Tunajua kuwa ni Mungu anayezilainisha roho za watu. Neno, hakika linatwambia katika Yohana kumi na mbili mstari wa thelathini na mbili, "nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu." Yesu atafanya sehemu yake nasi inabidi tuifanye sehemu yetu.

Mwisho, nataka kuwakumbusha kile ambacho Biblia inatwambia katika Mathayo sura ya nne, mstari wa kumi na tisa – Yesu anaongea na wanafunzi wake na anasema kuwa atakufanya mvuvi wa watu. Tupa ndani kama mkanda wa uvuvi, mstari huo wa maombi leo, ukiomba kuwa Mungu ataifungua milango ili watu zaidi waje kumjua Yesu Kristo ni nani kila mahali katika jumuiya zetu, kila mahali katika taifa letu, na kila mahali duniani. Sasa, niko tayari na najua uko tayari. Kwa hivyo tuombe.

## PASTOR KEITH FRITZ

Senior Pastor • Word of Faith Christian Center
Toronto, Canada

### Ombea Nguvu na Uvumilivu

Habari. Mimi ni Mchungaji Keith Fritz. Asante kwa kujiunga nasi katika siku zetu thelathini za maombi. Hii ni siku ya ishirini na nane na leo tunaomba kuhusu nguvu na uvumilivu.

Paulo alimhimiza Timotheo kupigana vita vilivyo vizuri vya imani; kushika uzima wa milele. Na kupigana vita hivyo vizuri vya imani, utahitaji nguvu na uvumilivu. Nguvu na uvumilivu hutoka kwa Mungu. Daudi anatambua pale nguvu yake hutoka. Zaburi hamsini na tisa, mstari wa tisa inasema, "Ee nguvu zangu, nitakungoja wewe, Maana Mungu ndiye aliye ngome yangu." Na halafu katika mstari wa kumi na sita anasema, "Nami nitaziimba nguvu zako,"

Paulo pia anatambua zinapotoka nguvu zake. Katika Wafilipi nne, mstari wa kumi na tatu, anasema, "Nayaweza mambo yote katika Kristo anitiaye nguvu." Na kwa nini tunaombea nguvu? Kwa sababu tunaweza kuwa wadhaifu. Wakorintho wa pili sura ya kumi na mbili, mstari wa tisa, Mungu akamwambia Paulo, "Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu." Neno nguvu hapo limetafsiriwa kuwa nguvu na uwezo. Nehemia sura ya nane, mstari wa kumi unasema, "Kwa kuwa furaha ya Bwana ni nguvu zenu." Nguvu hapa imetafsiriwa kuwa mahali pa usalama, ulinzi na kimbilio.

Je, mbona tunahitaji uvumilivu? Waebrania sura ya kumi, mstari wa thelathini na sita unasema, "Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi." Kwa hivyo, tunapotafuta kufanya mapenzi ya Mungu, na tunapomtegemea kwa nguvu na uvumilivu, tutapata kuwa Mungu amekuwa akifanya kazi yake kutufananisha na Kristo na kututayarisha kwa ajili ya baraka iliyoahidiwa. Omba kwa ajili ya nguvu na uvumilivu leo. Barikiwa.

## PASTOR LEE FERGUSON

Word of Faith Int'l Christian Center
Southfield, Michigan

### Omba kuhusu Mwamko Mkubwa wa Kiroho Duniani Kote

Jina langu ni Mchungaji Lee Ferguson na tutaongea kuhusu kuuombea mwamko mkubwa duniani kote. Katika Matendo ya Mitume nne, tukisoma kutoka mstari wa ishirini na tisa, inasoma, "Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako wa kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu." Kwa hivyo, ikiwa uko kama mimi na uko makini na mambo ya msingi unaweza kujua kuwa tunaishi wakati wa Timotheo wa pili inaposema kuwa wakati wa hatari utakuja. Tunaishi kihalisi katika nyakati za hatari sasa hivi. Ninavyoongea, kuna matangazo ya habari ya mashambulizi ya kigaidi dhidi ya taifa la Israeli na mamia ya watu wanauawa kwa mashambulizi ya kigaidi. Tunaona ripoti mbaya sana kuhusu ufyatuaji wa risasi katika shule zetu na vile kupitia mifumo ya elimu wanajaribu kuwafundisha watoto wetu mada na mazungumzo yaliyopotoka.

Kanisa lipo chini ya mashambulizi, chini ya kizuizi kila siku. Kuteswa kwa Wakristo kunafanyika kila siku. Tunaishi katika nyakati za hatari. Adui anapigana vita dhidi ya Mwili wa Kristo. Adui anapigana vita dhidi ya Mungu. Tunajua kuwa hawezi kushinda. Tayari amepoteza vita vyake. Hawezi kamwe kushinda dhidi ya Mwili wa Kristo. Hawezi kamwe kushinda dhidi ya Mungu. Lakini tuko hapa duniani tukiishi nyakati za hatari. Tunaishi kulingana na Maandiko.

Ni muhimu kuelewa kuwa njia pekee ya kukaa ndani ya ulinzi na kuwa na msingi wa kweli wa amani ni tunapotumia muda kwa maombi na tunapotumia muda kwa Neno Lake. Msingi wa pekee na wa kweli ambao tunao ni wakati tulipo kwenye uwepo wa Mungu. Tunaona kinachotendeka karibu nasi. Tunaona kinachotendeka katika habari zetu. Tunaona kinachotendeka katika jamii na jumuiya yetu, na dunia yetu. Lakini nataka kukuhimiza usizingatie kwa akili yako kile unachokiona bali uombee mwamko mkubwa utokee, sio tu kwa taifa hili, bali kwa dunia yote – mwamko mkubwa, nguvu ya Mungu ipenyeze jumuiya yetu, ipenyeze mji wetu, ipenyeze dunia yetu – kuwa nguvu ya Mungu, miujiza ya Mungu iweze kutimizwa na kuonekana kwenye maisha ya watu.


Unapofikiria kuhusu maisha yako na unapofikiria kuhusu watu walio karibu nawe, nataka ufikirie kuhusu na uweke akili yako ndani na uzingatie kuombea mwamko wa kiroho ufanyike katika familia yako, ufanyike katika nyumba yako, ufanyike katika kanisa lako, ufanyike katika shule zako, ufanyike katika chuo chako na kazini mwako – kuwa nguvu ya Roho Mtakatifu ipenyeze kwenye jamii yetu ili tuyaone macho ya vipofu yakifunguliwa, masikio ya viziwi yakifunguliwa, watu ambao hawawezi kutembea na wako kwenye viti vya magurudumu, waweze kuruka kutoka kwa viti vya magurudumu. Dunia inafaa kuona nguvu ya Mungu. Hilo litadhihirika pindi tu tutakapouchukua muda katika maombi na kwenye uwepo wa Bwana na kumuuliza Ajitoe mwenyewe kwa ulimwengu – Ili uweza wa Mungu utimie. Tunauhitaji sana mwamko wa kiroho. Tunaishi wakati ambao dunia inahitaji sana kuuona udhihirisho wa Roho Mtakatifu. Sisi tumekomaa. Tuko tayari kwa Bwana kudhihirisha kwa kweli nguvu Yake Duniani. Kwa hivyo usijalishwe na kile unachokiona. Usizingatie unachokiona. Lakini omba Maandiko. Omba kuwa Mungu atapenyeza dunia na nguvu Yake na kutakuwa na mwamko wa kiroho kwa taifa letu na kwa dunia yetu, katika jina la Yesu.

## BISHOP KEITH A. BUTLER

Senior Pastor and Presiding Bishop
Word of Faith Southfield, MI

### Omba utakavyoongonzwa na Roho Mtakatifu

Bwana asifiwe. Asante kwa kufanya kazi nasi katika siku thelathini za maombi. Mungu ameyasikia maombi yako. Anafanya kazi duniani kwa sababu yako kuwa tayari kuchukua muda wa kuwa mbele zake kwa niaba ya watu wengine na kwa niaba ya jamii yako. Daudi aliandika katika Zaburi sura ya ishirini na nane, mstari wa sita, "Na ahimidiwe Bwana, maana ameisikia sauti ya dua yangu." Mungu amezisikia dua zetu. Umefanya kazi fulani nzuri na maombi yako yanaleta mabadiliko sio tu kwa maisha ya watu wengi sana - utapata kuwa maombi yako yanaleta mabadiliko katika maisha yako binafsi na katika maisha ya familia yako. Mungu akubariki na asante kwa hilo katika jina la Yesu.




WORD OF FAITH INT'L CHRISTIAN CENTER
20000 W. 9 Mile Road • Southfield, Michigan 48075
PH: 248.353.3476 • Need Prayer: 800.541.7729
wordoffaith.cc

Bishop Keith A. Butler, Founder & Senior Pastor
Pastor MiChelle Ferguson, Executive Pastor